MUHTASARI WA KIKAO CHA 19 CHA KAMATI YA USHAURI YA MKOA WA RUKWA - (RCC) KILICHOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA OFISI YA MKUU WA MKOA (RDC) TAREHE 31/03/2010.

MAHUDHURIO:

WAJUMBE

1.	Mh. Daniel Ole Njoolay	- Mkuu wa Mkoa	- Mwenyekiti
2.	Bw. Salum M. Chima	- Katibu Tawala (M)	- Katibu
3.	Mh. Thobias M. Sijabaje	- Mkuu wa Wilaya SBA	- Mjumbe
4.	Mh. Joyce W. K. Mgana	- Mkuu wa Wilaya Nkasi	- Mjumbe
5.	Col. J. A. Mzurikwao	- Mkuu wa Wilaya Mpanda	- Mjumbe
6.	Mhe. Frank Mrema	- Meya - Manispaa ya SBA	- Mjumbe
7.	Mhe. David C. Ngalula	- Mwenyekiti wa H/W Nkasi	- Mjumbe
8.	Mhe. Alfred Mwanga	- Mwenyekiti wa H/W ya SBA	- Mjumbe
9.	Mhe. Philip J. Kalyalya	- Mwenyekiti wa H/W Mpanda	- Mjumbe
10.	Mhe. Yasini M. Katampa	- Mwenyekiti wa H/M Mpanda	- Mjumbe
11.	Bibi Sylivia Siriwa	- Mkurugenzi Manispaa SBA	- Mjumbe
12.	Bw. Benjamin O. B	- Kaimu Mkurugenzi H/W SBA	- Mjumbe
13.	Bw. Robert R. Mnkyalla	- K/Mkurugenzi H/W Nkasi	- Mjumbe
14.	Eng. Emmanuel Kalobelo	- Mkurugenzi H/W Mpanda	- Mjumbe
15.	Bw. Henry Haule	- Mkurugenzi wa Mji Mpanda	- Mjumbe

WASIOHUDHURIA:

1.	Mhe. Mizengo K. Pinda	- Waziri Mkuu na Mbunge Mpanda Mashariki	- Mjumbe
2.	Mhe. Dr. Chrisant Mzindakaya	- Mbunge Jimbo la Kwela	- Mjumbe
3.	Mhe. Ludovick Mwananzila	- Mbunge Jimbo la Kalambo	- Mjumbe
4.	Mhe. Said Arfi	- Mbunge Jimbo la Mpanda Kati	- Mjumbe
5.	Mhe. Elietta Switi	- Mbunge wa Viti Maalum (M)	- Mjumbe
6.	Mhe. Anna Lupembe	- Mbunge wa Viti Maalum(M)	- Mjumbe
7.	Mhe. P. P. Kimiti	- Mbunge Sumbawanga Mjini	- Mjumbe
8.	Mhe. Ponsiano D. Nyami	- Mbunge Jimbo la Nkasi	- Mjumbe
9.	Mhe. Abdallah Sumry	- Mbunge Jimbo la Mpanda Magharibi	- Mjumbe

WAALIKWA

(a) Wataalamu wa Sekretarieti ya Mkoa

1.	Bw. Elias M. Msafiri	- Katibu Tawala Msaidizi - Huduma za Utumishi na Utawala
2.	Bi. E. S. Mfinanga	- Katibu Tawala Msaidizi - Huduma za Jamii
3.	Bw. S. J. Mundia	- Katibu Tawala Msaidizi Huduma za Serikali za Mitaa
4.	Bw. W. J. Mnzava	- Kaimu Katibu Tawala Msaidizi Maendeleo ya Uchumi
5.	Bw. D. E. P. Kilonzo	- Kaimu Katibu Tawala Msaidizi Mipango na Uratibu
6.	Bw. K. Mahundi	- Kaimu Katibu Tawala Msaidizi - Miundombinu
7.	Bw. L. J. Kanoni	- Katibu Tawala Wilaya ya Mpanda
8.	Bw. S. Shillingi	- Katibu Tawala Wilaya ya Sumbawanga
9.	Bw. Josephat B. Kakuru	- Katibu Tawala Wilaya ya Nkasi
10.	Bw. A. M. Masse	- Mshauri Ustawi wa Jamii Sekretarieti ya Mkoa
11.	Bw. P. Mwandumbya	- Mwanasheria wa Sekretarieti ya Mkoa
12.	Dr. S. R. Kabuma	- Mganga Mkuu wa Mkoa
13.	Bw. Hamza Mvano	- Kaimu Mshauri Kilimo Sekretarieti ya Mkoa
14.	Bi. Emmy George	- Mhandisi Mshauri Maji Sekretarieti ya Mkoa
15.	Bw. Nicholaus Mchome	- Mshauri Maliasili /Mazingira Sekretarieti (M)
16.	Bw. Frank J. Maten	- Mshauri Maendeleo ya Jamii Sekretarieti (M)
17.	Bw. L. M. N Sesemkwa	- Mshauri wa Ushirika wa Sekretarieti (M)
18.	Bw. Mashalla Samson	- DPS wa Mkuu wa Mkoa
19.	Bw. Respich Maengo	- Kny Mshauri wa Mifugo Sekretarieti (M)
20.	Bw. G. O. Ouma	- Mshauri wa Teknohama Sekretarieti ya Mkoa
21.	Bw. F. Mtepa	- Katibu wa Hospitali ya Mkoa
22.	Bw. F. Chrisant	- Afisa Vijana wa Sekretarieti ya Mkoa
23.	Bw. F. P. Chonya	- Afisa Tawala wa Sekretarieti ya Mkoa
24.	Bw. M. Nzyungu	- Afisa Elimu - Taaluma
25.	Bw. Nestory, A. M.	- Afisa Elimu - Taaluma
26.	Bw. Nkenyenge M.	- Afisa Utamaduni na Michezo wa Sekretarieti ya (M)

27. Bw. Ocran B. Chengula - Afisa Kilimo wa Sekretarieti ya (M)
28. Bi. Devotha Mshumbusi - Afisa Uvuvi wa Sekretarieti ya (M)
29. Bw. Paul Nganyanyuka - Afisa Ushirika wa Sekretarieti ya (M)
30. Bi. Hawa Adam - Mtakwimu wa Sekretarieti ya (M)
31. Eng. Mashingia, E. J. - Afisa Kilimo wa Sekretarieti ya (M)
32. Bi. Schola Mbalila - Afisa Kilimo wa Sekretarieti ya (M)
33. Bi. Magreth Chipeta - Afisa Serikali za Mitaa wa Sekretarieti ya (M)
34. Bw. David Mlongo - Mwangalizi wa Ofisi
35. Bi. Halima Shillingi - Mtunza Kumbukumba Sekretarieti ya (M)
36. Bw. Harride A. Shimwela - Msaidizi wa Mtendaji wa Sekretarieti ya (M)
37. Bibi Daniella Leguna - Katibu Mahsusi Sekretarieti ya (M)
38. Bi. E. Malema - Katibu Mahsusi Sekretarieti ya (M)
39. Bi. H. Mbaule - Katibu Mahsusi Sekretarieti ya (M)
40. Bi. E. Moshi - Msaidizi wa Ofisi wa Sekretarieti ya (M)
41. Bi. D. Kyamba - Msaidizi wa Ofisi wa Sekretarieti ya (M)
42. Bw. Edgar Kasalama - Mhudumu wa Ofisi
43. Bw. T. J. Mwimanzi - TSD Rukwa

(b) Waalikwa toka Halmashauri za Wilaya

1. Bw. Martin Hamis - Misitu Sumbawanga
2. Bw. A. T. Wazabanga - Kaimu Afisa Elimu
3. Bi. Catherine Ulaya - Mratibu wa UKIMWI Manispaa ya Sumbawanga
4. Bw. Juma Mabrouk - Kaimu Afisa Utumishi Wilaya - Nkasi
5. Bw. A. M. Mwakabana - Afisa Mipango Wilaya - Nkasi
6. Bw. Dickson F. Mugaya - Kaimu Mtunza Hazina Wilaya - Nkasi
7. Bi. Kisoli T. A. - Kaimu Mtunza Hazina Wilaya - Mpanda
8. Bw. Mchina, G. S. - Kaimu Afisa Utumishi Wilaya - Mpanda Mji
9. Bw. Ferdinand Filimbi - Mchumi - Mpanda Mji
10. Bw. P. C. Kashindye - Kaimu Afisa Taaluma Manispaa ya Sumbawanga
11. Bw. Dankan S. Kipeta – Kaimu Mkufunzi Mkazi (TEWW)
12. Bw. Lupilya G. S. - Kaimu Mkurugenzi Manispaa ya Sumbawanga
13. Bw. Lazaro J. Bipa - Afisa Mipango - Sumbawanga Manispaa
14. Bw. Louis H. Chambi - Afisa Mipango – Sumbawanga (W)

15. Bw. Herbert Bilia - Afisa Mipango Msaidizi – Sumbawanga (W)
16. Bw. Issah Nzunda - Afisa Mipango – Mpanda Mji

(c) Waalikwa toka Chama Cha Mapinduzi

1. Mhe. H. Matete - Mwenyekiti wa CCM (M)
2. Bw. Kiwango, F. - Katibu wa CCM (M)

(d) Waalikwa toka Taasisi za Umma na Idara za Serikali

1. Bw. Martin Chang'a - Meneja SIDO (RUKWA)
2. Bw. A. M.G. Mukandara - Meneja - TRA
3. Bw. Mohamed Ntula - Kaimu Meneja wa TANROADS - Rukwa
4. Eng. Makala Hamisi - Kaimu Mkurugenzi Mtendaji - SUWASA
5. Bw. F. Ebenezer - Kaimu Afisa Usalama Mkoa Rukwa
6. Bw. Kanyengele K. - Mkufunzi mkazi Taasisi ya Elimu ya Watu wazima
7. Bw. Jacob Mwaruanda SSP - kny. Kamanda wa Polisi (M)
8. Bw. D. E. Kifanga - Mkaguzi wa nje (NAO)
9. Bw. Charles J. E. Ndumbaro - kny: Afisa Uhamiaji (M)
10. LT. Col. J.B Shayo - Mshauri Mgambo (M)
11. Bw. Louis W. Ndumbaro - Kaimu Afisa Mipango (MDC)
12. Bw. Athanas Y. Kikuji - NIC (T) Ltd.
13. Bw. T. J. Mwimanzi - Katibu TSD (M)
14. Bw. S. I. Kaisi - Meneja Uwanja wa Ndege
15. Bw. Sudi M. Kalonga - Idara ya Usalama wa Anga
16. Bw. Tweedsmvir Zambi - T.T.V. Regional Secr.
17 Bw. Joseph D. Wandi - WMA - Rukwa
18. Bw. Gerald Bwire - Kaimu Meneja Vipimo
19. Bw. Gabriel S. Hokororo - TAHOSSA Mkoa
20. Bw. W. R. M. Bambaganya - Afisa Uhamiaji Mkoa
21. Bi. Selina T. Mtakari - SSO – GPSA Rukwa
22. Bw. Denis Ndabirinde - HOST - Hazina Ndogo Rukwa
23. Bw. Makwinja Dismas Yusuf - Mkaguzi TASAF (M)
24. Bw. Crepinus A. Rwegasira - Meneja wa TTCL Rukwa
25. Eng. Joseph Nyamhanga - Meneja wa – TANROADS Rukwa

26. Eng. Alex R. Kimaro - Meneja wa – TEMESA Rukwa
27. Bw. F. Mtafya - Meneja SGR Rukwa

(e) Waalikwa toka NGOs, Mashirika ya Dini na Taasisi za Binafsi.

1. Bishop Jonas - Askofu wa Moravian Sumbawanga
2. Capt. Z. Noel Nkoswe - REMSO
3. Bw. Joel Amon - KAESO
4. Bw. E. M. Kinunda - Mwenyekiti TCCIA – Rukwa
5. Bw. Gaudence Kipesha - Mwenyekiti CATA
6. Bw. Issa Rubbega (Kidevu) - REYO
7. Bw. APE Msonda - Mwinjilisti/Mchungaji
8. Bw. Evod Kituta - Mwakilishi TADESO
9. Bi. Lydia Ruliho - M/Mwenyekiti MVIWATA Taifa
10. Sheikh Rashid Akilimali - Sheikh wa Mkoa
11. Bw. Alfred D. S. Mdegipala - Afisa Mtendaji TCCIA

(f) Waandishi wa Habari na Wapiga picha Walioalikwa

1. Bi. Juddy Ngonyani - Channel Ten/BTL
2. Bw. Peti Siyame - Mwandishi wa Habari Daily News
3. Bw. Mussa Mwangoka - Mwandishi wa Habari
4. Bw. Gurian Adolf - Mwandishi wa Habari
5. Bi. Irene Mwakalinga - Mwandishi wa Habari - TBC
6. Bw. Prosper Mgimwa - Mwandishi wa Habari
7. Bw. Oscar Simon - Mwandishi wa Habari - RFA

AGENDA NA. RCC 19/2010/1: KUFUNGUA KIKAO.

Mwenyekiti alifungua kikao kwa kuwakaribisha wajumbe wote na kuwapa pole ya safari kwa wajumbe waliotoka mbali, pia alitumia nafasi hii kuwataarifu wajumbe kifo cha Bw. Isack Masangula aliyekuwa Kaimu Katibu Tawala Msaidizi Kitengo cha Miundombinu aliyefariki usiku wa kuamkia tarehe 23/02/2010. Ndipo wajumbe walisimama kwa dakika moja kumwombea kwa Mungu ili aiweke roho yake mahali pema peponi - Amen.

Aidha Mwenyekiti alitoa pongezi za dhati kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kumteua Bw. Clement Lujaji aliyekuwa Katibu Tawala Msaidizi Kitengo cha Uchumi katika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa kuwa Katibu Tawala wa Mkoa wa Mara.

Pamoja na pongezi hizo Mwenyekiti alitaja mambo makuu manne (4) ambayo yamekuwa kikwazo kikuu cha maendeleo ya Mkoa wa Rukwa. Mambo hayo ni:-

1. Utekelezaji hafifu wa maagizo yanayotolewa katika vikao vyetu, aliendelea kukazia kuwa tunakaa vikao vingi na tunaagizana mambo mengi lakini utekelezaji haufanani na yale tuliyoongea na kukubaliana.

2. Fedha za miradi zinazotumika ni nyingi sana hasa katika Halmashauri, unapolinganisha thamani ya fedha iliyotumika inakuwa kubwa sana kuliko miradi inayojengwa.

3. Kutokamilika kwa miradi kama ilivyopangwa, alisema miradi mingi inachukua muda mrefu kukamilika na hata uwasilishaji wa taarifa nao umekuwa unachelewa. Mwenyekiti aliwaomba wajumbe kutekeleza majukumu yao kwa wakati.

4. Ufuatiliaji hafifu wa miradi au shughuli za Serikali watu wanafanya kazi mpaka wafuatiliwe wasipofuatiliwa kazi haifanyiki na bahati mbaya wataalam wanaotakiwa kufuatilia kazi za miradi na shughuli mbalimbali za Serikali hawafanyi hivyo na kwa hali hiyo hatuwezi tukapiga hatua katika kuleta maendeleo yaliyokusudiwa kwa Mkoa wetu. Aliwaomba wajumbe wote kubadilika kila mmoja atimize wajibu wake ipasavyo.

Baada ya kusema hayo Mwenyekiti alifungua kikao saa 4.20 asubuhi.

AGENDA NA. RCC 19/2010/2: *KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KIKAO CHA 18 CHA TAREHE 20/10/2009, PAMOJA NA KIKAO MAALUM CHA TAREHE 23 FEBRUARI 2010.*

Mwenyekiti aliwaongoza wajumbe kufanya masahihisho katika mihutasari yote miwili na masahihisho yalikuwa kama ifuatavyo:-

1. Ukurasa wa 12 neno “waalimu” lisomeke “walimu”
2. Ukurasa wa 19 neno “Sumbawanga Municipal” lisomeke “Sumbawanga Manispaa”
3. Ukurasa wa 11 wa Muhtasari wa kikao maalumu cha Ushauri cha Mkoa neno “Masangaula” lisomeke Masangula.
4. Ukurasa wa 12 neno “TANROAD” lisomeke “TANROADS”

Baada ya masahihisho hayo Kamati iliupitisha Muhtasari wa kikao Maalum na kikao cha 18 kuwa kumbukumbu sahihi za vikao vya Kamati ya Ushauri ya Mkoa vilivyofanyika tarehe 20/10/2010 na tarehe 23/02/2010.

AGENDA NA. RCC 19/2010/3: *YATOKANAYO NA KIKAO CHA TAREHE 20/10/2009 PAMOJA NA KIKAO MAALUM CHA TAREHE 23 FEBRUARI 2010.*

Mwenyekiti aliwaongoza wajumbe katika kupitia utekelezaji wa maazimio ya kikao cha 18 na kikao maalum cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa. Hata hivyo mambo yafuatayo yalijadiliwa katika agenda hii:-

1. Halmashauri ziondoe majibu ya kusema agizo hili limezingatiwa, liko kwenye mpango, agizo limetekelezwa au kusema mchakato unaendelea badala yake watoe takwimu sahihi zinazo jitosheleza.

2. Ilifafanuliwa kuwa uzoefu unaonesha watoto wa shule za msingi wakipata uji na chakula cha mchana mahudhurio yanaongezeka na kiwango cha kufaulu nacho kinaongezeka. Wakurugenzi waende wakashughulikie suala hili na kutoa takwimu sahihi za shule zinazotoa chakula.

3. Halmashauri zitunge sheria ndogo ndogo “by-laws” za kuwabana wazazi wachangie fedha ili watoto wa shule za msingi wapate uji na chakula cha mchana shuleni.

4. Ukurasa wa 13 wa Yatokanayo na Kikao cha 18 cha Kamati ya Ushauri neno “nyumba za walimu 583” lisomeke “nyumba za walimu 83”.

5. Kuongeza kasi ya ujenzi wa nyumba za walimu, ilielezwa kuwa hali ya ujenzi wa nyumba za walimu katika Manispaa ya Sumbawanga si wa kuridhisha ukilinganisha na Halmashauri nyingine.

6. Maeneo mengi ya mwambao hayana nyumba za walimu ndio maana walimu wengi wanakimbia maeneo hayo, kikao kiliagiza nyumba za walimu zijengwe katika maeneo hayo.

7. Mfuko wa watumishi uone uwezekano wa kutenga fedha kwa ajili ya kusomesha watoto yatima.

8. Mpango wa kutoa mafunzo kwa wakulima wagani uwe wa kudumu.

9. Vikundi vinavyopewa matrekta na “powertiller” vipewe mafunzo na elimu ya kutosha ili viweze kutumia vizuri “powertiller” na matrekta hayo kwani “powertiller” na matrekta mengi yaliyonunuliwa mwaka jana mengi yameharibika.

10. Kikao kilishauri kikundi kitakachoshindwa kutumia vizuri trekta au powertiller kinyang’anywe na kupewa kikundi kingine.

11. Maandalizi ya Nane Nane yaanze mapema na kila Halmashauri ipanie kushinda.

12. Kutoa msamaha kwa wazee wenye umri wa miaka 60 sambamba na kuandaa dirisha maalumu kwa ajili ya wazee utekelezaji ufanyike ndani ya

miezi miwili, ilipendekezwa mpaka tarehe 23/04/2010 agizo liwe limetekelezwa na siyo tarehe 23/05/2010 kama ilivyokuwa awali.

13. Suala la ukusanyaji wa mapato, Mwenyekiti aliipongeza Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda kwa ukusanyaji mzuri na kutoa onyo kwa Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi kwa ukusanyaji ulio chini ya kiwango, alitumia nafasi hii kuishauri Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi kwenda kujifunza mbinu zilizotumika kwa Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda.

AGENDA NA. RCC 19/2010/4: TAARIFA MBALIMBALI ZA UTEKELEZAJI KAZI.

(i) Taarifa ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya mwaka 2009/2010 kipindi kinachoishia 31 Disemba 2009.

Taarifa ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya mwaka 2009/2010 iliwasilishwa. Taarifa hii ilieleza kuwa katika mwaka wa fedha 2009/2010 mkoa wa Rukwa ulitengewa jumla ya sh.70,499,173,000/= kati ya hizo, fedha za mishahara zilikuwa shilingi 37,215,721,910/=, Matumizi ni shilingi 12,173,994,090/= na fedha za Maendeleo ni shilingi 21,109,457,000/=. Hadi kufikia mwezi Disemba 2009 jumla ya sh.46,078,025,011/= sawa na asilimia 65 zilikuwa zimekwisha pokelewa.

Ukusanyaji wa Mapato ya Halmashauri.

Katika mwaka wa fedha 2009/2010 Halmashauri za Wilaya, Mji na Manispaa za mkoa wa Rukwa zilikisia kukusanya jumla ya sh.2,743,000,959/=. Hadi mwezi Februari 2010 jumla ya sh. 1,982,794,737/= zilikuwa zimekusanywa sawa na asilimia 72 ya lengo la mwaka mzima.

Kamati ilipokea taarifa hiyo na kutoa pongezi kwa Halmashauri ya Mpanda kwa kukusanya kiasi cha asilimia 98 aidha kamati haikuridhishwa na ukusanyaji wa mapato uliochini ya kiwango katika Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi.

(ii) Taarifa ya utekelezaji wa Harakati za Mapambano dhidi ya VVU/UKIMWI kipindi kinachoishia 31 Disemba 2009.

Taarifa ya utekelezaji wa shughuli za UKIMWI iliwasilishwa na Mratibu wa UKIMWI wa Mkoa wa Sekta Mtambuka. Katika Taarifa yake alieleza kuwa kazi zilizofanyika kipindi kinachoishia 31 Disemba 2009 ni: Usimamizi na ufuatiliaji wa masuala ya UKIMWI, Kutoa hamasa ya mapambano ya UKIMWI kwa njia ya Sinema, Kuzijengea Uwezo Kamati za UKIMWI za Halmashauri, Kutoa elimu ya mapambano dhidi ya UKIMWI mahala pa kazi, Ununuzi na Usambazaji wa Kondomu, Maadhimisho ya Siku ya UKIMWI Duniani, Mafunzo kwa Waelimisha Rika, na Misaada kwa wahitaji.

Mtoa mada alieleza kuwa shughuli za mapambano dhidi ya UKIMWI kwa Mwaka wa fedha 2009/2010 zimetekelezwa kwa kiwango cha 69% hadi kufikia Machi, 2010. Fedha iliyotumika ni Tsh. 145,674,505 kati ya Tsh. 210,308,055 ambazo Mkoa ulipokea kwa ajili ya Mapambano dhidi ya UKIMWI.

(iii) Taarifa ya Mfuko wa Watumishi Mkoani Rukwa.

Taarifa ya utendaji na utekelezaji wa kazi za Mfuko wa watumishi iliwasilishwa. Taarifa hii ilieleza kuwa katika kipindi cha mwaka 2009/2010 mfuko ulijipangia kufanya kazi kuu nne:-

- Kubuni mbinu zaidi za kutafuta fedha toka kwa wanachama na wadau wa mfuko na kukusanya ahadi za michango ambazo mfuko uliahidiwa kwenye harambee na kujenga kitega uchumi ndani ya Manispaa ya Sumbawanga.
- Kuwatafuta na kutoa motisha kwa watumishi wapya wa Idara ya Afya na Elimu walio nje ya Mkoa ili waje wafanye kazi mkoa wa Rukwa.
- Kujitangaza zaidi kwa wananchi wote na kuhamasisha kuchangia/kutoa kiasi fulani cha mchango ili kuwezesha mfuko wa watumishi kupanua wigo na kusomesha watoto yatima na walio kwenye mazingira hatarishi.
- Kufanya mikutano na wadau wa mfuko ili kupata maoni yao juu ya katiba ya mfuko na kuajiri Mtendaji Msaidizi wa mfuko.

Mratibu wa Bodi ya mfuko alieleza kuwa shughuli za mfuko zilizofanyika kipindi cha Julai 2009 mpaka Machi 2010 ni:-

- Bodi ya Mfuko tayari imepitisha mpango wa kujenga kitega uchumi na juhudi za kutafuta kiwanja zinaendelea. Mtendaji wa Mfuko tayari amemwandikia barua Mkurugenzi wa Manispaa kuomba kiwanja cha kutosha majibu yanasubiriwa kiwanja kikipatikana kazi itaanza mara moja.

- Katika kutafuta watumishi wapya na kutoa motisha Mfuko umeshawishi na kutoa motisha kama ifuatavyo:

a) Walimu wa Stashahada (Diploma) 97 walipewa motisha ya Sh.150,000/= awamu ya kwanza na awamu ya pili watapewa baada ya miezi mitatu.

b) Walimu wa Shahada (Digrii) 123 walipewa motisha ya Sh.300,000/= awamu ya kwanza na awamu ya pili itatolewa ili kulinda mali za mfuko. Idadi hiyo ni nje ya ile ya walimu wa sayansi 24 walioletwa Agosti 2009. Hivyo jumla kuu ya walimu wa Shahada ni 147 hadi kufikia tarehe 31/03/2010.

c) Mpaka sasa tumefanikiwa kuleta Manesi 28 na Waganga Wasaidizi wawili (2) kwa gharama ya milioni 19, watumishi hawa bado wanaendelea kuja kulingana na wanavyomaliza kozi zao vyuoni.

- Bodi ya mfuko imetenga sehemu ya michango ya Harambee kwa ajili ya kuchangia katika ujenzi wa miundombinu ya Elimu hasa kwenye ujenzi wa Hosteli za wasichana kwa kutoa bati bandali kumi (10) kwa Halmashauri baada ya Mkurugenzi husika kuomba kwa Mwenyekiti wa Bodi ya Mfuko. Tayari mfuko umekabidhi bandali 10 kwa Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga kwa ajili ya ujenzi wa Hosteli ya wasichana Kasanga Sekondari.
- Mfuko utajenga Hosteli ya wasichana kwenye shule ya sekondari Kizwite yenye thamani ya Sh. 50,000,000/= ambayo ni ahadi ya Mamlaka ya Elimu Tanzania.

- Bodi ya Mfuko imepitisha Mpango wa kuanza kuchangia kiasi fulani cha fedha katika kusomesha watoto yatima. Fedha hii ni ile itakayotokana na faida ya hisa/gawio ambazo wamewekeza UTT. Kila Halmashauri itatoa idadi sawa ya watoto yatima wa kusomeshwa na mfuko ambapo mchakato wa kutambua watoto yatima wanaostahili kusaidiwa utafanywa na sekretarieti ya mfuko na viongozi wa kata husika na huenda kila kata itatoa mtoto wa kusaidiwa.

- Katika kuanza kusomesha watoto yatima Mfuko umepata mfadhili ambaye amekubali kumgharamia mtoto yatima wa kike kuanzia kidato cha kwanza hadi kidato cha sita. Sekretarieti ya mfuko, Maafisa Elimu wa Halmashauri chini ya Afisa Elimu wa Mkoa waliendesha mchakato wa kumpata mwanafunzi wa kike anayeitwa Judith Dismas kutoka shule ya sekondari Chisenga iliyoko Kasanga. Kutokana na ushauri wa Mfadhili na Watendaji wa mfuko wamekubaliana ahamishiwe katika shule ya sekondari ya ST.Theresia iliyopo Manispaa ya Sumbawanga. Gharama ya kumsomesha kwa mwaka ni takribani shilingi 800,000/=. Mfadhili ataingiza fedha kwenye akaunti ya shule na mfuko utaletewa “Pay-in-slip” ya benki.

Kikao kiliipokea taarifa hii na kuipitisha. Aidha kikao kiliagiza mfuko utafute mtu wa fani ya uchumi ambaye ataweza kubuni na kutafuta vyanzo vya mapato na anayeweza kuandaa na kubuni miradi kwa ajili ya mfuko. Pia Halmashauri ziliagizwa kuendelea kuchangia mfuko wa watumishi ili mfuko uendelee kuwa hai.

(iv) Taarifa ya mwaka 2009 ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi Mkoani Rukwa kipindi kinachoishia 31 Disemba 2009.

Taarifa iliyowasilishwa ilihusisha kazi zilizofanyika katika Halmashauri 5 za Mkoa wa Rukwa na Sekretarieti ya Mkoa. Taarifa hii ilikuwa imeandaliwa na kukamilika mwezi Disemba 2009, na kuwasilishwa kwa Katibu Mkuu OWM-TAMISEMI kwa barua yenye Kumb. Na. FA. 187/195/01/45 ya tarehe 14 Januari 2010. Aidha taarifa hizi zilikuwa zimepitiwa na vikao vya kisheria vya Halmashauri zote na Kamati za Ushauri za Wilaya (DCC) ambapo zilijadiliwa

na kutolewa ushauri kwa ajili ya kuboresha utekelezaji ili kuondoa kero za wananchi kwa kasi zaidi.

Kikao kilielezwa kuwa, taarifa hii pia ilipitiwa na kujadiliwa katika kikao cha Halmashauri kuu ya CCM ya Mkoa wa Rukwa tarehe 06/01 2010, ambapo Chama Cha Mapinduzi kiliipongeza Serikali na kutoa Maoni na ushauri na mapungufu yaliyojitokeza katika kikao hicho na yalifanyiwa marekebisho.

(iv) Taarifa ya utekelezaji wa shughuli za Huduma za Jamii kuanzia Julai - Disemba 2009.

Taarifa ya utekelezaji wa shughuli za Huduma za Jamii iliwasilishwa ambapo ilielezwa kuwa tarehe 09 – 10/09/2009 wanafunzi wa darasa la saba walifanya mtihani wa kumaliza elimu ya Msingi. Jumla ya watahiniwa 30,777 wakiwemo wavulana 15,794 na wasichana 14,983 walisajiliwa kufanya mtihani. Watahiniwa 13,571 sawa na asilimia 47.60% wakiwemo wavulana 8,218 na wasichana 5,353 walifaulu mtihani, wanafunzi Raia waliochaguliwa awamu ya kwanza walikuwa 8,902 kati ya 12,680 ya waliofaulu sawa na 65.7%. Kati yao wavulana 5,160 na wasichana 3,742. Wanafunzi 3,778 sawa na 42.43% walikosa nafasi wakiwemo wavulana 2,482 na wasichana 296.

Baada ya awamu ya kwanza ya uchaguzi, Halmashauri zilifanya jitihada za kuongeza nafasi za kidato cha kwanza kwa kufanya yafuatayo:-

(i) Kuongeza mikondo
(ii) Kuongeza vyumba vya madarasa kwa kujenga vyumba vipya katika baadhi ya shule
(iii) Kujenga na kufungua shule mpya.

a) Wanafunzi waliosajiliwa kufanya Mtihani wa kumaliza Elimu ya Msingi Mwaka 2010.

Ilielezwa kuwa jumla ya watahiniwa 22,004 wamesajiliwa mwaka 2010 kati yao 14,326 ni wavulana na 13,678 ni wasichana aidha wamo watahiniwa wa MEMKWA 136 ambapo wavulana ni 75 na wasichana ni 61.

b) Taarifa ya utekelezaji wa shughuli za Elimu ya Sekondari.

Mtaalam alieleza kuwa Mtihani wa kidato cha nne ulifanyika tarehe 05 – 23/10/2009 na kidato cha pili mwezi Novemba 2009. Majedwali yafutayo yanaonesha takwimu za matokeo hayo.

Matokeo ya Kidato cha Nne Mwaka 2009.

Halmashauri	Waliopata									Waliofanya Mtihani
	DIV.I	DIV. II	DIV. III	JML	%	DIV. IV	%	DIV. 0	%	JUMLA
Mpanda (M)	4	17	64	86	15.7	318	58.6	140	25.7	543
Mpanda (V)	1	22	78	101	13.7	478	68.9	158	17.4	737
Nkasi	0	8	32	40	5	465	57.6	302	37.4	807
S'wanga (M)	25	38	194	257	18	880	61.8	288	20.2	1425
S'wanga (V)	4	28	103	135	11.2	843	69.8	229	19.0	1207
JUMLA	**34**	**113**	**471**	**618**	**13.1**	**2984**	**62.2**	**1117**	**23.7**	**4719**

Matokeo ya Kidato cha Pili Mwaka 2009.

Idadi ya Shule	Waliofanya Mtihani	Wasiofanya Mtihani	Waliopata							
			A	B	C	D	JUMLA	%	F	%
91	8622	824	5	304	2441	3116	5866	68.0	2756	32

c) Taarifa ya utekelezaji wa shughuli za Michezo na Utamaduni.

Sekta ya Utamaduni na Michezo ipo chini ya Kitengo cha Huduma za Jamii katika Sekretarieti ya Mkoa. Majukumu ya Sekta hii ni pamoja na kujishughulisha na Maendeleo ya Michezo na Utamaduni kwa wafanyakazi na wananchi kwa ujumla wakiwemo wanafunzi, walimu na vijana kupitia mamlaka husika. Shughuli za Michezo na Utamaduni zilizofanyika ni pamoja na:

(a) Kuandaa na kupeleka timu kushiriki katika mashindano ya Wizara na Idara za Serikali (SHIMIWI) 2009 yaliyofanyika Mkoani Morogoro, kuanzia tarehe 17/10/2009 hadi 04/11/2009. RAS Rukwa Sports Club, ilikuwa na jumla ya wachezaji 38 waliounda timu sita (6), Netball, Football, Kuvuta kamba, Draft na Bao. Kwa ujumla timu zetu zilifanyika vizuri kwa kuonesha upinzani na hasa ukichukulia ilikuwa mara yao ya kwanza kushiriki, hii ilitia moyo sana.

(b) Ofisi imefuatilia na kusambaza nakala za nyaraka muhimu zinazohitajika katika utendaji wa Wilaya zote kutoka Wizara na Idara husika. Hii ikiwa ni hatua ya kuwapa uelewa zaidi washikadau kuhusu haki na wajibu wao.

(c) Timu za Mpira wa miguu zipatazo 26 zimesajiliwa ikiwa ni Mpanda timu nane (8) na Sumbawanga timu 18. Pia Vyama viwili (2) na Klabu tatu (3) zimesaidiwa kutengeneza Katiba.

(d) Ofisi imefanya ufuatiliaji wa maeneo ya kihistoria yaliyohifadhiwa katika Halmashauri na kupata takwimu za maeneo hayo. Ushauri umetolewa kwa Wakurugenzi, Maofisa Utamaduni kuhusu kusaidiwa kutimiza lengo hilo kwa ajili ya faida ya vizazi vijavyo.

(e) Viwanja vya shule mbalimbali za Sekondari vimekaguliwa katika Halmashauri za Mpanda Mji na Mpanda Vijijini. Hali halisi ni kuwa bado viwanja havikidhi viwango vya ubora kwani havina alama za vipimo na pia nyasi ni nyingi hasa kipindi cha mvua pamoja na kukosa magoli (football, netball na volleyball)

d) Taarifa ya utekelezaji wa shughuli za Ustawi wa Jamii.

Huduma za Ustawi wa Jamii ziliendelea kutolewa katika Halmashauri tano za mkoa wa Rukwa yaani Mpanda (W), Mpanda Mji, Nkasi (W), Sumbawanga (W) na Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga. Hadi sasa Halmashauri ambazo zimeajiri Maofisa Ustawi wa Jamii ni tatu ambazo ni Mpanda (W), Nkasi (W) na Manispaa ya Sumbawanga.

Kazi zilizofanyika:

- Kusuruhisha na kushauri ndoa hamsini (50) zenye migogoro.
- Ushauri umetolewa kuhusu matunzo ya familia ishirini (20)
- Watoto yatima waliotambuliwa ni KE 5944 + ME 2863 = 3081. Kazi hii inaendelea ili kupata takwimu halisi katika makundi maalum.
- Jumla ya walemavu wa ngozi (Albino) 61 KE 31 ME 30 walitambuliwa.

e) Idara ya Afya.

Sekta ya Afya imeendelea kuimarika licha ya matatizo ya upungufu mkubwa wa rasilimali, pamoja na mila na desturi za wakazi kupenda zaidi tiba asilia kuliko tiba za kisasa. Matatizo haya yamesababisha Mkoa kutofikia haraka malengo yaliyokusudiwa. Kufuatana na ikama Mkoa ulitakiwa kuwa na watumishi wenye ujuzi 2,915, lakini ni watumishi 728 tu ndio waliopo kwa sasa.

Wakazi wa Mkoa huu wanahudumiwa na Hospitali nne (4), vituo vya Afya 31 na Zahanati 199. Kwa ujumla hali ya huduma ya afya ni mbaya hasa kwa vijiji vya pembezoni ambako wafanyakazi wanaokubali kwenda huko ni wachache sana.

Changamoto zilizopo.

(a) Imani potofu katika jamii
(b) Miundo mbinu mibovu
(c) Usafiri na usafirishaji
(d) Uchakavu wa majengo
(e) Uhaba wa watumishi
(f) Mzigo wa magonjwa
(g) Magonjwa yanayozuilika kwa chanjo
(h) Huduma ya chanjo

- **Mwongozo wa utoaji wa huduma za Matibabu kwa Wazee.**

Mkoa wa Rukwa una wazee wenye umri wa miaka 60 na zaidi wapatao 60,000 sawa na asilimia nne (4) ya watu wote. Katika maisha ya kijadi wazee na vijana wamegawana majukumu, wazee ni walinzi wa mila na desturi, washauri/wapatanishi na walezi wa watoto wadogo. Ilielezwa kuwa takwimu zinaonesha magonjwa yanayowasumbua sana wazee ni:-

- Sonana (Depression)
- Kupoteza kumbukumbu (Memory problem)
- Delirium
- Shinikizo la Damu (Hypertension)
- Kisukari (Diabetes mellitus)
- Kansa ya kibofu na tezi la mkojo

- Kansa ya kizazi na maziwa
- Magonjwa ya mifupa
- Magonjwa ya mfumo wa fahamu
- Utapiamlo
- Matatizo yatokanayo na kukosa matunzo

Kutokana na magonjwa haya kuwa ya muda mrefu na yanayohitaji gharama kubwa Mkoa umeamua kuandaa mwongozo utakaowezesha wazee kupata tiba. Hivyo utaratibu wa kuwatambua wazee ufanyike kwa kuanzia ngazi ya kijiji hadi Wilaya, utaratibu huo utafanyika kama ifuatavyo:

- Vijiji kuwatambua wazee wote walio na umri wa miaka 60 na zaidi ambao hawana uwezo wa kipato na kupeleka taarifa zao kwenye ngazi ya Kata ambako nao watapeleka Wilayani.
- Wilaya itandaa vitambulisho kwa ajili ya Tiba ya wazee. Wilaya Itafanya utambuzi wamahitaji ya wazee, kutoa ulinzi na matunzo.
- Mkoa utasimamia utoaji wa huduma na kuzihimiza Halmashauri za Wilaya zitoe na ziboreshe huduma kwa wazee.

Kamati ilipokea na kuipongeza taarifa hii. Aidha wajumbe walizitahadhalisha Halmashauri za Wilaya za Sumbawanga vijijini na Manispaa ya Sumbawanga kwa kuwaacha wanafunzi wengi waliofaulu darasa la saba kwa sababu ya kutojenga vyumba vya kutosha vya madarasa. Pia wajumbe walishauri Maafisa Ustawi wa Jamii wasimimie na kutatua tatizo la watoto wa mitaani ambao wamekuwa wengi sana hasa katika Manispaa ya Sumbawanga.

AGENDA NA. RCC 19/2010/5: MPANGO WA MWAKA 2010/11-2012/13.

(i) Mpango Mkakati wa Sekretarieti ya Mkoa "Revised Rukwa Region Secretariat Strategic Plan" wa mwaka 2010/11-2012/13.

Mjumbe alieleza kuwa umuhimu wa Mpango Mkakati ni kuwajulisha wadau wetu mambo ambayo Sekretarieti ya Mkoa inatarajia kuyafanya katika miaka 3 ijayo. Aidha Mpango Mkakati wa Mkoa unaelezea sisi ni nani, tunafanya nini na jinsi tutakavyotimiza malengo tuliyojiwekea. Mpango mkakati huu wa

miaka 3 kuanzia mwaka 2010 hadi 2013 umeandaliwa baada ya kuisha muda kwa mpango mkakati uliopita ambao uliandaliwa mwaka 2006/2007 na kuishia mwaka 2008/09. Mpango huu unahuisha Mpango wa awali kwa kuzingatia mazingira mapya yanayoikabili Sekretarieti ya Mkoa. Mabadiliko ambayo yamejitokeza kati ya mwaka 2006 na 2010 ambayo yanasababisha kuhuisha mpango wa awali na kuandaliwa kwa mpango mpya ni haya yafuatayo:-

- Kumalizika kwa kipindi cha utekelezaji wa mpango mkakati wa mwaka 2006/2007 hadi 2008/2009.
- Kuwepo kwa muundo Mpya wa Sekretarieti za Mkoa.
- Kuongezeka kwa majukumu ya Sekretarieti za Mkoa na wadau wake, kutokana na ugatuaji wa madaraka “Decentralisation by Devolution – D by D”.
- Kuwepo kwa Sheria, Sera na Kaulimbiu mpya kama vile Kilimo Kwanza.

Namna Mpango Mkakati ulivyoandaliwa:

Mpango Mkakati wa Mkoa umeandaliwa kwa njia shirikishi kwa kuhusisha uongozi wa juu na watendaji wengine. Mpango huu pia ni matokeo ya marejeo kutoka Mpango Mkakati wa Kati “Medium Term Strategic Planning”. Dira ya Taifa ya Maendeleo; Mwongozo wa Bajeti, Ilani ya Uchaguzi ya Chama Tawala; Mkakati wa Taifa wa kupunguza umaskini na sera nyingine za Kitaifa.

Mpangilio wa Mpango Mkakati wa Sekretarieti ya Mkoa.

Mpango Mkakati wa Sekretarieti ya Mkoa umegawanyika katika sura nne (4) kama ifuatavyo:-

- Sura ya 1 - Utangulizi
- Sura ya 2 - Uchambuzi wa Hali Halisi “Situation Analysis”
- Sura ya 3 - Mpango wenyewe
- Sura ya 4 - Matokeo tarajiwa.

Kikao kilipokea na kutoa shukrani za dhati kwa wote waliohusika katika kuundaa Mpango Mkakati wa Sekretarieti ya Mkoa.

(ii) Bajeti na Mpango wa Maendeleo Mkoani kwa mwaka 2010/11-2012/13.

Taarifa ya Bajeti na Mpango wa Maendeleo Mkoani Rukwa iliwasilishwa. Katika taarifa hiyo ilielezwa kuwa katika kuandaa Mpango na Bajeti ya mwaka 2010/2011, Mkoa umezingatia maeneo ambayo Serikali imeyaweka wazi na kuyapa kipaumbele kwa kupitia mwongozo ulioandaliwa na kutolewa kwetu na Wizara ya Fedha kuhusu viwango vya ukomo na vipaumbele vya bajeti kwa mwaka 2010/2011 - 2012/2013. Aidha Mkoa umezingatia pia Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005, Sera mbalimbali za Taifa na Kisekta, Dira ya Maendeleo 2025, MKUKUTA, Malengo ya Milenia (MDGs), Dhana ya Serikali ya **Kilimo Kwanza** na Maagizo ya kitaifa kuhusu kuimarisha mapinduzi ya kilimo. Mpango huu pia umezingatia vipaumbele vya Mkoa wa Rukwa ambavyo ni Miundombinu, Kilimo, Elimu, Maendeleo ya Watumishi, Mazingira, Maji, Afya & UKIMWI na SACCOS.

Mwelekeo wa Mkoa kwa mwaka ujao wa fedha wa 2010/2011.

i Kukamilisha utekelezaji wa Mpango wa Utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2005 kwa kipindi cha 2005 – 2010.

ii Kuendelea kutekeleza majukumu ya msingi ya Sekretarieti ya Mkoa na Halmashauri zake.

iii Kutoa tafsiri sahihi ya sera mbalimbali za serikali kwa matumizi ya Halmashauri, taasisi, asasi na mashirika yasiyo ya serikali mkoani na kuendelea kutekeleza maelekezo yote yanayotolewa na Serikali katika ngazi zote.

iv Kuratibu mipango mbalimbali ya maendeleo ya kijamii na kiuchumi katika Mkoa.

v Kusimamia utekelezaji wa Mpango mkakati wa MAKIRU (Mapinduzi ya Kilimo Rukwa) na KILIMO KWANZA kama shughuli kuu na mpango pekee unaoweza kuwaongezea kipato wakazi wa Mkoa huu na kuwaondolea umaskini.

vi Kuandaa taarifa mbalimbali za maendeleo ya kijamii na kiuchumi kwa matumizi ya wadau mbalimbali Mkoani na Taifa kwa ujumla.

MAKADIRIO YA MWAKA 2010/2011.

Mkoa wa Rukwa katika kipindi cha mwaka **2010/2011** unaomba kuidhinishiwa kiasi cha Shilingi **88,430,178,680/=** kwa ajili ya kutekeleza programu mbalimbali zilizopangwa kufanyika katika ngazi ya Sekretarieti ya Mkoa na Serikali za Mitaa. Kati ya kiasi hiki, Shilingi **40,822,792,247/=** ni kwa ajili ya Mishahara, Shilingi **14,150,562,300/=** kwa ajili ya Matumizi ya kawaida na kiasi cha Shilingi **33,456,824,133/=** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

Katika kipindi cha mwaka 2010/2011; Sekretarieti ya Mkoa wa Rukwa imekadiria kutumia kiasi cha Shs**. 7,885,809,000/=** ambapo kiasi cha Sh. **2,482,803,000/=** ni kwa ajili ya Mishahara, Sh. **3,295,000,000/=** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Sh. **2,108,006,000/=** ni kwa ajili ya shughuli za Maendeleo, fedha za Ndani ni Sh. **1,540,113,000/=** na fedha za Nje ni Sh. **567,892,596/=**

Mamlaka ya Serikali za Mitaa katika Mkoa wa Rukwa, zimekadiria kutumia kiasi cha Sh. **80,544,369,680/=;** kati ya kiasi hiki, Sh. **38,339,989,247/=** ni kwa ajili ya Mishahara (PE); Sh. **10,855,562,300/=** kwa ajili ya matumizi kawaida (OC) na Sh. **31,348,818,133/=** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

(ii) Mpango wa Mkakati wa kupambana na maambukizi ya VVU/UKIMWI Mkoani Rukwa kwa mwaka 2010/2011 - 2012/2013.

Mpango mkakati

Mtoa mada alianza kuwasilisha kwa kuwajulisha wajumbe kuwa Mpango Mkakati unawasilishwa kwao kwa kuwa Kikao hiki ni cha Wadau wa Mkoa hivyo wanatakiwa wachangie kwa kutoa ushauri na maoni ili kuuboresha kabla Mpango haujawasilishwa Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS) kwa hatua zaidi. Aliendelea kusema kuwa Mipango Mikakati ngazi ya Halmashauri imekamilika kwa kuhusisha Wadau wote na ipo tayari.

Wajumbe walijulishwa kuwa Mpango Mkakati wa UKIMWI ni wa Wadau wote na utatumiwa kama mwongozo katika mapambano dhidi ya UKIMWI. Aidha, maeneo manne ya Kimkakati yaliainishwa ambayo ni: Kinga, Matunzo na Tiba, Mazingira Wezeshi na Misaada kwa Wahitaji.

Wajumbe walijulishwa kuwa Malengo ya Mpango Mkakati ni kushusha kiwango cha maambukizi ya UKIMWI cha sasa 4.9% na kukabiliana ipasavyo na athari zote ambazo Mkoa umezipata kutokana na Janga la UKIMWI. Mtoa mada alihitimisha kwa kuelezea kuwa tathmini ya utekelezaji wa Mpango Mkakati huu itafanyika kila baada ya mwaka mmoja na matokeo ("Impact") yatapimwa baada ya miaka mitatu.

Baada ya kuwasilisha Wajumbe walipitisha Mpango Mkakati wa kupambana na maambukizi ya VVU/UKIMWI wa Mkoa.

(iii) Mpango Mkakati wa kudhibiti Maafa na Majanga Mkoani Rukwa wa mwaka 2010/2011 - 2012/2013.

Mtaalam aliwasilisha Mpango Mkakati wa kudhibiti Maafa na Majanga Mkoani Rukwa. Taarifa hiyo ilieleza kuwa majanga ambayo yamekuwa yakiukabili Mkoa wetu ni:

(i) **Vimbunga** - Historia inaonesha kuwa Mkoa umekuwa ukikumbwa na vimbunga mara kwa mara. Wilaya ambazo zimekuwa zikikabiliwa na majanga ya vimbunga ni Sumbawanga, Nkasi na Mpanda.

(ii) **Magonjwa ya mlipuko:**

Magonjwa ya mlipuko yamekuwa yakiukumba Mkoa wetu mara kwa mara. Magonjwa haya ni kipindupindu na Surua.

(iii) **Ajali za vyombo vya usafiri:**

Hizi ni ajali za nchi kavu na majini. Ajali hizi zimekuwa zikipoteza maisha ya watu wengi katika Mkoa wetu. Ajali nyingi za vyombo vya usafiri zimekuwa zikitokea katika vyombo vinavyosafiri katika ziwa Tanganyika.

(iv) **Mafuriko** - Mkoa umekuwa ukikumbwa na majanga ya mafuriko katika maeneo ya mabondeni hasa yale yaliyo karibu na Ziwa Tanganyika na bonde la Ziwa Rukwa. Tarafa zinazokabiliwa na mafuriko mara kwa mara ni za Kirando na Karema.

(v) **Wadudu, wanyama waharibifu na magonjwa ya mifugo:** Kumbukumbu zinaonesha kuwa majanga ya wadudu, wanyama waharibifu na magonjwa ya mifugo yamekuwa yakijitokeza mara kwa mara. Katika Mkoa wetu tumekuwa tukikumbwa na wadudu waharibufu ambao ni nzige wekundu. Mkoa wetu una sehemu mbili ambazo ni mazalia ya nzige hao wekundu. Maeneo hayo ni Iku/Katavi na bonde la Ziwa Rukwa.

(vi) **Radi** - Mkoa wa Rukwa umekuwa ukikumbwa na radi mara kwa mara. Radi hizi zimekuwa zikisababisha uharibifu wa majengo na vifo kwa wakazi wa Mkoa wetu. Katika Mkoa wetu Wilaya ya Nkasi inaongoza kwa matukio ya radi ikifuatiwa na Wilaya ya Sumbawanga.

(vii) **Moto** - Wananchi wa Mkoa wetu wamekuwa wakikumbwa na majanga ya moto ambayo yamekuwa yakisababisha uharibifu wa majengo na mali. Aidha Mkoa pia umekuwa ukikumbwa na tatizo la uchomaji moto kwa maeneo ya misitu na kuathiri wanyama na mimea ya asili katika maeneo yanayochomwa. Hili limekuwa ni tatizo la Wilaya zote za Mkoa wetu.

(viii) **Matetemeko ya Ardhi** - Mkoa wetu umepitiwa na bonde la ufa tawi la Magharibi, hivyo Mkoa wetu upo katika hatari ya kukumbwa na matetemeko ya ardhi japo katika Mkoa wetu hakuna rekodi ya tetemeko lililosababisha maafa.

Kikao kiliipokea taarifa hii na kuagiza viwekwe vizuia radi na vifaa vya kuzimia moto (“Fire Extinguishers”) sehemu za taasisi na maeneo ya mkusanyiko mkubwa wa watu.

(iv) Mpango wa utekelezaji wa Ilani ya uchaguzi Mkoani Rukwa wa mwaka 2010 kipindi cha Januari-Disemba 2010.

Mpango wa utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi wa mwaka 2005, uliotekelezwa katika kipindi cha kuanzia Januari hadi Disemba 2009, uliwasilishwa. Mpango huo uliandaliwa katika Halmashauri za Mkoa wa Rukwa na kuunganishwa ili kupata mpango wa utekelezaji wa Ilani wa Mkoa ambapo tarehe 20 Januari 2009 ulikuwa umekamilika na kuwasilishwa kwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI kwa barua yenye Kumb. Na. FA.187/195/01.

Kwa vile mpango huu umeunganishwa kutoka katika ngazi za Halmashauri, na kupitiwa na kujadiliwa katika vikao vya kamati za Ushauri vya Wilaya, Mabaraza ya Madiwani ya Halmashauri, pamoja na vikao za Halmashauri Kuu za CCM za wilaya husika ambako wajumbe wengi wa kikao hiki ni wajumbe katika vikao hivyo, tunaamini wajumbe walipata nafasi ya kutosha ya kutoa ushauri juu ya mapungufu yaliyokuwepo.

Wajumbe waliipokea taarifa hii kwa kauli moja na kuitakia serikali katika ngazi zote, utekelezaji mzuri wa mpango huo.

AGENDA NA. RCC 19/2010/6: MENGINEYO KWA IDHINI YA MWENYEKITI.

Mwenyekiti aliendelea na agenda ya mengineyo kwa kusema kuwa alipokea hoja kutoka kwa wajumbe wanne na kuomba kila mmoja kuwasilisha hoja yake.

1. **Maombi maalum ya Fedha ya Shilingi 2,668,532,000/= ya Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga.**

Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga aliwasilisha maombi maalum kwa ajili ya kutengeneza Barabara ya Kalambazite - Kasamvu - Ilemba na Daraja la Chombe ambalo liliharibika kutokana na mvua nyingi, mchanganuo wa matengenezo hayo ni kama ifuatavyo:

- Matengenezo Barabara ya Kalambazite – Kasamvu - Ilemba (km 24) **Sh.2, 377,182,000/=.**

- Ujenzi wa daraja la Chombe **Sh.291, 350,000**/=. Baada ya maelezo hayo wajumbe walipitisha maombi hayo.

2**.** Maombi maalum ya Fedha za DADPS kutoka Sh.207, 208,000/= hadi Sh. 600,000,000/= ya Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga.

Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga aliwasilisha maombi maalum ya kuomba kuongezewa fedha za DADPS kutoka **Sh.207,208,000/= hadi kufikia Sh. 600,000,000/=** kutokana na ukweli kuwa Halmashauri hiyo ina jumla ya Vijiji 25 vinavyoizunguka Manispaa na wakazi wengi wa eneo hilo ni wakulima, hivyo Halmashauri inahitaji fedha za kutosha ili kuweza kujenga Vituo vya Habari vya wakulima, kununua trekta kubwa na "powertillers" kwa ajili ya kuwasaidia wakulima pamoja na kuendeleza miundombinu ya Umwagiliaji. Baada ya maelezo hayo wajumbe waliipokea taarifa.

3. Hoja ya Katibu wa CCM (M).

Katibu wa CCM (M) aliwasilisha Hoja zifutazo:

- Barabara ya Namanyere - Ninde ilifungwa bila ya wananchi kupewa taarifa na hivyo kusababisha tatizo kubwa la mawasiliano. Je Serikali ina mpango gani?

  Jibu - Barabara ya Namanyere – Ninde iliibuliwa na wananchi kupitia mpango wa TASAF. Fedha zilizotolewa hazikutosha kukamilisha barabara hiyo hasa daraja, hivyo kwa mwaka wa fedha wa 2010/2011 zimetengwa Sh. 10,000,000/= toka "Road Fund" na Sh.87, 836,542/= ambazo ni 'special request' zimeombwa toka Hazina ili kukamilisha daraja hilo.

- Zahanati ya Kizumbi iliungua moto na Mganga kuondolewa bila kukabidhi dawa kwa kamati ya afya. Je nini hatma ya afya za wananchi?

  Jibu: Katika mwaka wa fedha wa 2010/2011 Zahanati ya Kizumbi inatakiwa kujengwa upya kutokana na maafa yaliyotokea. Gharama za ujenzi zitajulikana baada ya tathimini kufanyika.

- Wananchi wa familia mbili Kirando walifyekewa mahindi yao na raia wakorofi. Kesi inasuasua Mahakamani na hivi sasa hawana chakula. Je Serikali inalishughulikiaje tatizo hilo?

  Jibu: Mkuu wa Mkoa ameidhinisha fedha kwa ajili ya kununua gunia nne (4) za mahindi na kilo mia moja (100) za maharage ili kusaidia familia hizo mbili (2) kupitia Mfuko wa Maafa.

4. Hoja ya Mwenyekiti wa REYO.

Mwenyekiti wa REYO alitoa hoja kuwa anayo miche mingi ya matunda katika bustani yake, hivyo anawakaribisha wajumbe wote kuchukua miti hiyo kwa ajili ya kupanda katika maeneo mbalimbali. Mkuu wa Mkoa alitoa agizo kuwa kwa vile tarehe 01/04/2010 ni siku ya kupanda miti, basi ichukuliwe miche 1,000 na kupanda katika maeneo mbalimbali.

5. Utekelezaji wa kazi za Maji.

Mwenyekiti aliagiza Meneja wa SUWASA atoe taarifa ya utekelezaji wa kazi za maji katika kikao kijacho cha kamati ya ushauri ya mkoa.

AGENDA NA: RCC 19/2010/7: KUFUNGA KIKAO.

Mwisho Mwenyekiti alifunga kikao mnamo saa 8.30 mchana kwa kuwasisitiza wajumbe kwenda kutafakari na kutekeleza maagizo yote yaliyotolewa. Baada ya hayo aliwatakia wajumbe utekelezaji mwema.

UMETHIBITISHWA

_____	_____
Daniel Ole Njoolay	Salum Mohamed Chima
MWENYEKITI	**KATIBU**

Tarehe_____